



GRETCHEN WHITMER
GOVERNOR

STATE OF MICHIGAN
OFFICE OF THE GOVERNOR
LANSING

GARLIN GILCHRIST II
LT. GOVERNOR

AGIZO LA UTENDAJI

No. 2020-15

Idhini ya muda ya ushiriki wa mbali wa mikutano ya hadhara, masikilizo na msaada wa muda mfupi unaohitajika kwenye mikutano ya mwezi ya bodi za shule

Virusi vya Corona (COVID-19) ni virusi vinavyoathiri mfumo wa upumuaji unaoweza kusababisha kuumwa mahututi au kufa. Virusi hivi vinasababishwa na mlipuko wa virusi vya corona ambavyo hapo kabla havikuwahi kutambuliwa kwa binadamu na ni rahisi kuenezwa kutoka mtu mmoja kwenda mwingine. Mpaka sasa hakuna chanjo au tiba ya kuzuia ugonjwa huu.

Mwezi Machi 10, 2020, Idara ya Afya na Huduma za Binadamu ilitambua kesi mbili zilizobainika kuwa na maambukizi ya COVID-19 hapa Michigan. Siku hiyo hiyo, nilitoa Agizo la Mtendaji 2020-4. Agizo hili lilitangaza hali ya dharura jimbo zima la Michigan chini ya kifungu cha 1 cha ibara ya 5 ya Katiba ya Michigan ya mwaka 1963, na Sheria ya usimamizi wa Dharura ya mwaka 1976 PA 390, kama ilivyorekebishwa, MCL 30.401-.421, na mamlaka ya sheria ya Gavana ya mwaka 1945, 1945 PA 302, kama ilivyorekebishwa, MCL 10.31-.33

Usimamizi wa Sheria ya Dharura inampa mamlaka yenye nguvu na majukumu kukabili(ana) na hatari kwenye jimbo hili au watu wa jimbo hili kupatwa na maafa au dharura” ambapo gavana anaweza kuitekeleza kupitia “agizo la utendaji, matangazo, na maelekezo yenye nguvu na manufaa kisheria” MCL 30.403(1)-(2). Vivyo hivyo Sheria ya Dharura yenye nguvu ya Gavana ya mwaka 1945, inaeleza, baada ya gavana kutangaza hali ya dharura, “gavana anaweza kutoa amri ifaayo, kanuni, na utekelezaji wa sheria kwa kuangalia manufaa itakayolinda maisha na mali au kuweza kudhibiti hali ndani ya eneo lililoathirika.” MCL 10.31(1).

Ili kupunguza maambukizi ya COVID-19, kulinda afya ya jamii, na kutoa kinga kwa wananchi wa Michigan walio hatarini, ni muhimu sana kwa wananchi wa Michigan kuchukua tahadhari zitakazoweka mipaka ya uwepo binafsi ya watu kukutana. Hizi njia muhimu za upunguzaji zinajumuisha kukaa mbali na kuweka mipaka ya idadi ya watu kuwepo kwenye mikutano ya hadhara.

Mwisho, ni sahihi na lazima kusitisha kwa muda kanuni na taratibu zinazohusiana na uwepo wa mtu kimwili mikutanoni na masikilizo ya baraza la umma na vyombo vyote vya serikali ya Michigan. Vyombo hivi vya umma lazima viendeleo kufanya shughuli za umma wakati huu wa dharura, pamoja na hatua ya kuwajibika kwenye COVID-19, na jamii kwa ujumla lazima iendeleo kushiriki kwenye maamuzi ya serikali bila kuhatarisha kabisa afya ya jamii, usalama na ustawi.

GEORGE W. ROMNEY BUILDING • 111 SOUTH CAPITOL AVENUE • LANSING, MICHIGAN 48909
www.michigan.gov
PRINTED IN-HOUSE

Kupitia Katiba ya Michigan ya mwaka 1963 na Sheria ya Michigan, natoa maagizo yafuatayo:

1. Kuanzia sasa na kuendelea mpaka Aprili 15, 2020 11.59 jioni, kwa kiwango cha Sheria ya mikutano ya wazi, 1976 PA 267, kama ilivyorekebishwa, MCL 15.261 kwenda 15.272 (“OMA”) inayotaka mikutano ya baraza la umma kufanyika sehemu za watu kuwepo maeneo husika au inataka uwepo wa kimwili wa mtu mmoja au wawili wa baraza la uma, kufuata kwa umakini kifungu cha 3 cha OMA, MCL 15.263, kimesitishwa kwa muda ili kiweze kupunguza haja ya uwepo kimwili wa mtu, kama ifuatavyo:
 - (a) Mikutano ya baraza la umma inaweza kufanywa kwa njia ya kielektroniki, pamoja na njia ya kongamano la simu au njia ya kongamano la video, kwa namna ambayo wananchi kwa ujumla na wanachama wa baraza la umma wanaweza kushiriki kutumia njia ya kielektroniki.
 - (b) Mkutano wa baraza la umma unaofanyika kielektroniki lazima ufanywe kwa njia-mbili ya mawasiliano ili wanachama wa baraza la umma waweze kusikia na kusikilizwa na wanachama wengine wa baraza la umma na pia washiriki wa umma kwa ujumla wawasikie wanachama wa baraza la umma na pia kusikilizwa na wanachama wa baraza la umma na washiriki wengine wakati wa kipindi cha maoni kwa umma. Baraza la umma linaweza kutumia teknolojia kuwezesha kuchapa maoni ya umma ambayo yanaweza kusomwa au kushirikishwa na wanachama wa baraza la umma na washiriki wengine.
 - (c) Ushiriki wa wanachama wa baraza la umma na umma kwa ujumla mikutanoni kwa njia ya kielektroniki inazingatiwa kuwa ni ya uwepo wa mahali husika na ushiriki wao ni kama wako kwenye mikutano husika kwa uwepo wa kimwili.
 - (d) Watu wote lazima waruhusiwe kushiriki kwenye mkutano wowote wa baraza la umma kielektroniki isipokuwa itolewavyo tofauti na OMA
 - (e) Ikiwa baraza la umma linaendesha moja kwa moja au sio moja uwepo rasmi wa mtandao, baraza la umma lazima, kwa uthabiti na nyongeza ya mahitaji ya taarifa zinazokubalika chini ya OMA, litume mapema taarifa ya mkutano utakaofanyika kielektroniki kwenye sehemu ya tovuti ya shirika la umma ambayo inapatikana kikamilifu na umma. Taarifa ya umma kwenye tovuti lazima iwekwe kwenye ukurasa wa nyumbani au kwenye ukurasa tofauti wa tovuti uliotengwa kwa ajili ya matangazo ya umma yasiyokuwa na ratiba maalumu ya mikutano ya umma au mikutano ya kielektroniki na ipatikane kwenye kiunga kinachojulikana na ieleze dhahiri kwenye tovuti ukurasa wa nyumbani kwa uwazi dhumuni lake kwa ajili ya kuarifu mikutano hiyo ya kielektroniki au isiyo kuwa na ratiba maalumu. Taarifa ya mkutano wa baraza la umma litakalofanywa kielektroniki lazima lijumuishe haya yote yafuatayo:
 - (i) Ieleze sababu ya shirika la umma kufanya mikutano kwa njia ya kielektroniki.

- (ii) Zieleze umma kwa kina taratibu ambazo umma unaweza kutumia ili uweze kushiriki kwa njia ya kielektroniki, iambatanishe namba za simu, barua pepe au hivi vyote kwa pamoja.
 - (iii) Taratibu ambazo watu wanaweza kuwasiliana na wanachama wa umma ili kutoa maoni au kuuliza maswali ya biashara yoyote itakayojitokeza kwenye mkutano wa shirka la umma
 - (iv) Taratibu ambazo watu wenye ulemavu wanaweza kushiriki mkutanoni.
- (f) Haki ya mtu ya kushiriki katika mkutano wa baraza la umma uliofanyika kielektroniki ni pamoja na haki ya kurekodi mkanda, kuchukua video, kutangaza moja kwa moja maendeleo ya mkutano wa hadhara kwenye vyombo vya habari na televisheni. Walakini, baraza la umma linaweza kuanzisha sheria na kanuni zinazofaa ili kupunguza uwezekano wa kuvuruga mkutano.
- (g) Baraza la umma halina masharti ya kumzuia mtu asishiriki mikutano ya hadhara inayofanyika kielektroniki kujiunga au vinginevyo kutoa jina lake au maelezo mengine au vinginevyo kutimiza masharti ya kuhudhuria, mbali na taratibu za lazima za kumruhusu mtu kushiriki wakati wa kutoa maoni ya hadhara kwenye mkutano.
- (h) Mtu lazima apate ruhusa ya kutoa hotuba kwenye mikutano ya hadhara ya kielektroniki chini ya kanuni zilizoundwa na kuhifadhiwa na baraza la umma. Mtu hatakiwi kutengwa kwenye mkutano utakaofanyika kielektroniki isipokuwa kama uko wazi kwa umma kuvunja amani wakati wa mkutano.
- (i) Wakati wa mkutano wa baraza la umma lililofanyika kwa njia ya kielektroniki, wanachama wa umma walihimizwa kupiga kura zote kwa kuita majina kuepukana na maswali kuhusu namna wanachama wote wanavyopiga kura.
- (j) Iwapo baraza la umma linafanya mkutano kielektroniki moja kwa moja au sio moja kwa moja kwa uwepo wa mtandao, baraza la umma linashauriwa kutangaza ajenda kwenye mtandao rasmi wa tovuti kupitia ukurasa wa nyumbani na nyenzo nyingine zinazohusu mkutano huo.
- (k) Vinginevyo wanachama wa umma wanaoshiriki kwenye mkutano wa umma uliofanywa kielektroniki wanaweza kutengwa wasishiriki kwenye kipindi cha siri cha baraza la umma kilichofanywa kielektroniki, wakati wa mkutano huo kama kipindi cha siri kinakutana na kinafanyika kwa kufuata matakwa ya OMA yanayokubalika na kipindi cha siri.
2. Baraza la umma lifanyalo mkutano kielektroniki kama ilivyo chini ya agizo hili linashauriwa kufanya hivyo kwa njia inayowezakana kikamilifu kwa dhumuni la OMA, inayojumuisha kukuza uwajibikaji wa serikali na kukuza uwazi wa serikali na kuongeza kufanya maamuzi sahihi ya kimsingi. Majadiliano au mazungumzo kwenye mkutano wa wazi ambao hayawezi kwa kiwango cha chini kusikilizwa na ushiriki wa umma kwa ujumla kwenye mkutano ni kinyume na madhumuni haya. Ipasavyo, wanachama wa baraza la serikali lazima waupuke kutumia barua pepe, kutumia ujumbe wa simu wa maandashi, ujumbe wa kielektroniki wa hapo hapo, na


njia nyingine za mfumo wa kielektroniki kufanya maamuzi au kukusudia kwenye kufanya maamuzi, na lazima kuepuka maamuzi ya “pande zote” kwa njia ambayo haiwafikii umma kwenye mkutano wa wazi.

3. Kama amuzi au hatua nyingine za baraza la umma linafuata matakwa ya agizo hili na matakwa ya OMA, basi imepitishwa na OMA.
4. Kuanzia sasa na kuendelea mpaka Aprili 15, 2020 11:59 jioni, kama sheria nyingine au agizo ambalo sio la OMA linahitaji maoni ya umma kuruhusiwa au kusikilizwa kwa umma, pamoja na idhini ya kutoa kibali au usikilizwaji kwa matakwa ya chini ya Sheria Bajeti na Utaratibu wa Uhasibu, 1968 PA 2, kama ilivyorekebishwa, MCL 141.421 kwenye 141.440a, baraza la umma au Idara au shirika linaweza kutoa njia ya maoni ya umma kwa uwepo wa mbali au ushiriki kupikia matumizi yoyote ya kielektroniki ambayo yatamwezesha mwanachama wa umma kwa ujumla uwezo wa kushiriki akiwa mbali kwa kiwango ambacho hakina tofauti na uwepo wake binafsi. Ikiwa haikutolewa idhini ya wazi ya sheria au amri, maoni ya maandishi, ijumuishayo njia ya kielektroniki, pia inaruhusiwa.
5. Kuanzia sasa na kuendelea mpaka Aprili 15, 2020 11:59 jioni, kibali kikali kwenye kifungu kidogo cha 6 cha sehemu ya 11a, kifungu kidogo cha 7 cha sehemu ya 384, na kifungu kidogo cha 1 cha sehemu 418a Msimbo wa shule uliorekebishwa, 1976 PA 451, kama ilivyorekebishwa, MCL 380.11a(6), MCL 380.384(7), na MCL 380.418a(1), kimesimamishwa kwa muda ili bodi za wilaya ya shule sizihitajike kufanya mikutano angalau mara moja kwa mwezi.
6. Hakuna kinachozuia kwenye agizo hili baraza la umma kuweka mipaka au kuzuia haki ya habari au vyombo vya habari vingine. Wanachama wa mabaraza ya umma wanashauriwa kuwezesha upatikanaji wa maandishi wa habari na vyombo vya habari vingine kwenye mikutano yote inayofanyika kielektroniki na kwa wanachama wamabaraza ya umma.
7. Kama ilivyotumika katika agizo hili, neno “uamuzi”, “mkutano”, na “baraza la umma” maana ya maneno hayo yamefafanuliwa chini ya kifungu cha 2 cha OMA, MCL 15.262, isipokuwa agizo hili halihusu mabaraza ya kutunga sheria ya serikali.
8. Kipengele cha agizo hili kiko juu ya kipengele gonganishi chochote cha mamlaka husika, kanuni au sheria.
9. Agizo hili linachukua nafasi ya kifungu cha 2 na 3 ya Maelekezo ya Utendaji 202-2

Imetolewa chini ya sahihi yangu na Muhuri Mkuu wa Jimbo la Michigan

Tarehe: Machi 18, 2020

Wakati: 4:46 jioni



GRETCHEN WHITMER
GAVANA

Kutoka kwa Gavana:

KATIBU WA JIMBO